# KWA KUWA SASA UMEOKOKA

**(Muongozo wa mafundisho na maombi kwa waongofu wapya)**

**PASTOR TONY OSBORN**

**© July 2024 Pastor Tony Osborn**

Kitabu hiki kimeandikwa na **PASTOR TONY OSBORN**. Haki zote zimehifadhiwa, huruhusiwi kunakili, kurudufu au kutumia sehemu ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi.

Kufanya hivyo itakuwa ni ukiukwaji wa taratibu na hii inaweza kukupelekea kushtakiwa kutoka kwa waandaaji wa kazi hii.

**Pastor, Tony Osborn**

**Dar es salaam, TANZANIA (Afrika Mashariki)**

**Simu: 0762153539/0659085731**

**Instagram / Tiktok: Pastor Tony Osborn**

**ISBN: 978-9912-9872-9-6**

# YALIYOMO:


**SHUKRANI: ........................................................................ vi**

**UTANGULIZI: ...................................................................... viii**

**Sura ya 1:**

**MAANA YA KUOKOKA ............................................................ 1**

1.1 MAANA YA KUZALIWA MARA YA PILI ........................................ 1

KINACHOZALIWA MARA YA PILI NI NINI? ................................ 2

1.2 BAADA YA KUOKOKA NINI HUTOKEA? ..................................... 3

1.3 KWANINI NI MUHIMU KUOKOKA? ............................................ 4

1.4 NINI KINATOKEA MTU AKIOKOKA? .......................................... 5

**Sura ya 2:**

**YAKUPASAYO KUFANYA BAADA YA KUOKOKA ........................ 8**

2.1 KUFUNGA ............................................................................ 8

2.2 KUOMBA ............................................................................. 11

2.3 KUSOMA NENO ..................................................................... 14

2.4 MARAFIKI NA WATU SAHIHI ................................................... 15

2.5 KUHUDHURIA IBADA .............................................................. 15

2.6 YASIYOKUPASA KUFANYA BAADA YA KUOKOKA ............. 16

2.7 HATUA ZA UKUUAJI ............................................................. 19

MTU AFANYE NINI ILI APATE KUKUA KIROHO? .................. 21

2.8 AHADI ZA MUNGU MAISHANI MWAKO BAADA YA KUOKOKA ........................................................................... 23

**Sura ya 3:**

**KUJAZWA ROHO MTAKATIFU NA FAIDA ZAKE ..................... 25**

Roho Mtakatifu ni nani? ........................................................... 25

3.1 FAIDA ZA ROHO MTAKATIFU KATIKA MAISHA YETU ..... 26

3.2 KUNENA KWA LUGHA NINI? .................................................. 27

FAIDA ZA KUNENA KWA LUGHA NI ZIPI? .............................. 27

3.3 NIFANYE NINI KAMA SIWEZI KUNENA KWA LUGHA MPYA? .............................................................................. 29

3.4 NAMNA YA KUPAMBANA NA HOFU NA MASHAKA ........... 29

**Sura ya 4:**

**MAJARIBU BAADA YA KUOKOKA ................................................ 31**

4.1 KUILINDA IMANI YAKO .......................................................... 34

*Unawezaje kuilinda imani yako?* ................................................................. 34

**Sura ya 5:**

**MUONGOZO WA MAOMBI YA ULINZI NA UTAWALA WA KILA SIKU ............................................................................ 37**

**HITIMISHO .................................................................................... 46**

**MAELEKEZO NAMNA YA KUTUMA SADAKA YAKO NA KUJIUNGA NA PARTNERSHIP ...................................................... 47**

# SHUKRANI:

Ninamshukuru Mungu sana kwa uaminifu wake na kwa kunijalia ROHO MTAKATIFU ambaye kwa mafunuo yasiyo ya kawaida amenipa NEEMA ya kuandika kitabu hiki ambacho kitakuwa muongozo wa mafundisho na maombi kwa wote waliompokea Yesu.

Mwanangu moja ya maamuzi mazuri zaidi uliyowahi kufanya tangu unazaliwa ni; "Kumpokea Yesu kuwa Bwana na mwokozi wa maisha yenu." na kamwe hutokuja kujutia maamuzi haya uliyoyachukua ya kuokoka.

Shukrani zangu za pekee ziwafikie watoto wangu wa kiroho wote, ndani na nje ya nchi ya Tanzania, kwa kunipenda, kuniombea na zaidi ya yote kunipokea na kuniamini na kumuamini Mungu aliyeniita na huduma iliyopo ndani yangu. Ninawashukuru sana kwa kuwa nyie mmenipa nafasi katika mioyo yenu na kuamini huduma ambayo Mungu ameiweka ndani yangu.

Kwa waongofu wapya na wasomaji wote, ahsanteni kwa kuchagua kusoma kitabu hiki. Maoni yenu na shauku yenu ya kukua kiroho ni chachu iliyoniwezesha kuweka juhudi zangu zote katika kuandika mwongozo huu. Ni matumaini yangu kwamba kitabu hiki kitakuwa msaada mkubwa kwenu katika safari yenu mpya ya imani.

Ninawapenda, ninawaombea na Mungu wa mbinguni awabariki sana.

Kiupekee kabisa ninamshukuru mke wangu mpenzi Mrs Neema Tony Kapola ambaye amekuwa akikesha pamoja nami, akisukuma na kusimamia kwa ufasaha ukamilifu wa kitabu hiki. Ninakupenda na Asante kwa kusimama na mimi katika wito na kazi hii ambayo Mungu amenipa.

Mwisho, napenda kutoa shukrani kwa timu ya wachapishaji na wahariri ambao wamefanya kazi kwa bidii kuhakikisha kitabu hiki kinakuwa bora na kinawafikia wasomaji kwa ubora wa juu. Mchango wenu ni wa thamani sana na unathaminiwa mno.

Asanteni sana kwa wote. Mungu awabariki na kuwazidishia hekima na baraka zake. Mungu aendelee kukuonekania wewe na familia yako ndani ya mwaka huu.

Kwa Upendo na Shukrani,

**[Pastor Tony Osborn]**

# UTANGULIZI:

Karibu kwenye kitabu hiki chenye jina la **"KWA KUWA SASA UMEOKOKA"** (Muongozo wa mafundisho na maombi kwa waongofu wapya). Nina furaha kubwa kukuletea mwongozo huu muhimu ambao umelenga kusaidia wale wote ambao wamechukua hatua ya imani na kumkubali Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wao.

Wokovu ni hatua ya kwanza muhimu katika safari ya kiroho ya Mkristo. Hata hivyo, baada ya kuokoka, waongofu wapya mara nyingi hukumbana na changamoto nyingi na maswali mengi kuhusu jinsi ya kuishi maisha mapya ya Kikristo. Kitabu hiki kimetayarishwa kwa makusudi ya kutoa mwongozo wa kina kwa waongofu wapya ili kuwasaidia kukua kiroho, kuelewa msingi wa imani yao, na kujenga msingi imara wa maisha yao mapya ndani ya Kristo.

Katika kurasa zijazo, utapata mafundisho ya msingi ya Kikristo yanayohusisha:

Imani na Maadili ya Kikristo: Mwongozo wa hatua kwa hatua juu ya mafundisho muhimu ya imani ya Kikristo.

Maombi:Mifano ya maombi ya kila siku itakayokusaidia kuimarisha uhusiano wako na Mungu.

Maisha ya Kikristo: Jinsi ya kuishi maisha ya ushindi na ushuhuda wa kweli katika jamii yako.

Kwa kupitia mwongozo huu, ni matumaini yangu kuwa utapata nguvu na ujasiri wa kuendelea katika safari yako ya kiroho, ukijua kuwa hauko peke yako. Mungu yupo pamoja nawe, na jamii ya waamini iko tayari kukusaidia na kukuunga mkono.

Nakukaribisha uingie kwa shauku na moyo wazi, ukijua kuwa hiki ni mwanzo wa safari ya ajabu. Mungu akubariki na akuongoze katika kila hatua ya maisha yako mapya ya wokovu.

SURA YA 1:

# MAANA YA KUOKOKA

Kuokoka ni kukombolewa na kuhamishwa kutoka kwenye utumwa wa maisha ya dhambi na mateso ya nguvu za giza. Ni kutolewa kutoka kwenye milki ya ufalme wa shetani na kuingizwa kwenye ufalme wa Bwana Yesu.

**“Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza kwenye ufalme wa mwana wa Pendo lake, ambaye katika Yeye tuna ukombozi yaani msamaha wa dhambi” (Wakolosai 1:13-14.)**

Lakini maana nyingine ya kuokoka ni kuzaliwa mara ya pili katika utu wa mtu wa ndani, yaani nafsi na roho yake kwa kufanywa upya. Kwanini kufanywa upya mara pili? Kwasababu kipindi mtu alipokuwa katika maisha ya dhambi, yaani kuishi katika ufalme wa shetani, utu wa mtu wake wa ndani uliharibiwa hata kufa. Hivyo pindi mtu anapokubali kuzaliwa mara ya pili, Mungu humfufua na kumzaa upya kutoka katika mauti na kumpa uzima wa utu wake wa ndani.

Neno linasema;

**“Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zetu. Ambazo mliziendea zamani kwa kuifuata kawaida yaulimwengu huu, na kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi… Lakini Mungu kwa kuwa ni mwingi warehema kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda, hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu alituhuisha pamoja na Kristo, yaani mmeokolewa kwa neema” (Waefeso 2:1-2,4-5.)**

## 1.1 MAANA YA KUZALIWA MARA YA PILI

Kuzaliwa mara ya pili ni tendo la kiroho linalohusisha kufanywa upya kwa nafsi na roho ya mtu kupitia neno la Mungu, ambalo ni mbegu. Kama vile ambavyo mwili wa mwanadamu unavyotengenezwa kwa

mbegu ya mwanamume anapokutana kimwili na mwanamke hata mtu kupata kuzaliwa, ndivyo ilivyo neno la Mungu ambalo ni mbegu linalotamkwa na Mungu na mtu akalisikia na kuliamini katika moyo wake ndipo nafsi na roho ya mtu hufanywa upya na kumpata mtu aliyezaliwa mara ya pili. Pia kuzaliwa mara ya pili ni kufanywa upya kwa maisha ya mtu kupitia mbegu isiyoharibika ambayo mbegu hiyo ni neno la Mungu.

Neno linasema;

**"Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili si kwa mbegu iharibikayo bali kwa ile isiyoharibika, kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele" (1 Petro 1:23.)**

**KINACHOZALIWA MARA YA PILI NI NINI?**

Kinachozaliwa mara ya pili ni nafsi na roho ya mwanadamu, au kwa lugha nyingine ni utu wa ndani wa mwanadamu. Tunapoongelea nafsi ni mjukumuiko wa akili, hisia na maamuzi na tunapo ongelea roho ni uhai unaoipa nguvu nafsi ya mwanadamu kuishi katika mapenzi ya Mungu na kufanikiwa.

**"Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi akampulizia puani pumzi ya uhai, mtu akawa nafsi hai" (Mwanzo 2:7)**

Katika neno la Mungu ambalo tumesoma, tumeona Mungu alipomuumba mwanadamu aliweka uzima katika utu wake wa ndani ambao baada ya kuanguka katika dhambi kwa adamu na hawa huo uzima uliondoka hivyo mtu wa ndani akawa amekufa katika roho na kuwa hai katika mwili.

**"Roho ndiyo itiayo uzima, mwili haufi kitu. Maneno hayo niliyowaambia ni roho tena ni uzima" (Yohana 6:63.)**

Kwanini kinachozaliwa mara ya pili ni nafsi na roho? Kwa sababu huyo ndiyo mtu halisi anayeishi ndani ya mwili na kusababisha matukio yanayoendelea au kutokea mwilini. Hivyo kwa kuzaliwa mara

ya pili kwa nafsi na roho maana yake kila tendo litakalokuwa linafanyika mwili litakuwa limebeba mapenzi ya Mungu.